



Jukwaa la Malengo ya Jiji la Albuquerque mwaka 2022

Baada ya kila miaka minne, wanajamii huunganika pamoja ili kutoa michango yao kuhusu malengo ya kimkakati ya Jiji la Albuquerque na hali za jamii zinazopendelewa. Kushiriki kwako ni muhimu kwa ubunifu wa hali ya baadaye ya Albuquerque. Jiunge nasi katika mojawapo ya matukio haya ili utoe mchango wako.

- Alhamisi, tarehe 22 Septemba saa kumi na mbili jioni (6:00 pm). Central & Unser Library Community Room, 8081 Central Ave NW 87121.
TAFADHALI JIBU MWALIKO HAPA: bit.ly/3wBZEpn. Huduma ya ukalimani itapatikana kwa zaidi ya lugha 100 kwa njia ya simu.
- Jumamosi, tarehe 1 Oktoba saa nne unusu asubuhi (10:30 am). International District Library Community Room, 7601 Central Ave NE 87108.
TAFADHALI JIBU MWALIKO HAPA: bit.ly/3wzCKPI. Huduma ya ukalimani itapatikana kwa zaidi ya lugha 100 kwa njia ya simu.
- Jumanne, tarehe 4 Oktoba saa kumi na mbili jioni (6:00 pm) kwenye Zoom kupitia kiungo cha bit.ly/3TfwO89. Huduma ya ukalimani wa lugha ya Kihispania itapatikana.

Unaalikwa pia kutoa mchango wako mtandaoni wakati wowote kuanzia Jumatano, tarehe 14 Septemba hadi Ijumaa, tarehe 7 Oktoba katika abqgoals.com. Huduma ya tafsiri inapatikana katika fomu hii ya mtandaoni.

Tukio la Jukwaa la Malengo huandaliwa na shirika la Indicators Progress Commission (IPC), wakazi kumi na wawili wa kujitolea walioleuliwa na Meya kwa ushauri na idhini ya Halmashauri ya Jiji.

Shirika la IPC linawajibika kwa kupendekeza marekebisho ya maono ya Jiji, malengo na hali za jamii zinazopendelewa. Washiriki kwenye Jukwaa la Malengo wana jukumu muhimu kwa kueleza hali ya baadaye ya Albuquerque ambayo wangependa kuona.

Mbinu hii ya kutoa mchango bora inawapa maafisa waliochaguliwa na viongozi wa jamii mkondo muhimu wa kufuata wanapo jitahidi kubuni hali ya baadaye ya Albuquerque. Unaweza kuona maono ya sasa ya Jiji, malengo na hali zinazopendelewa, na hatua zilizopigwa ili kuzitimiza katika cabq.gov/ipc.